Pia Sheria imetoa katazo la kusafirisha mnyama ambaye ni mgonjwa au ambaye amezaa ndani ya saa arobaini na nane.

### 3. Kuchinja wanyama

Katika kuchinja mnyama Sheria imeweka mazingira ya ulinzi wa wanyama pale anapotaka kuchinjwa kuwepo na mazingira ambayo siyo ya mateso au kwa kutumia kifaa maalumu katika kuchinja kwa kuzingatia mazingira na afya ya mnyama. Mtu yeyote haruhusiwi kuchinja mnyama ambaye ana mimba isipokuwa kwa sababu isiyozuilika ya kuthibiti ugonjwa.

### 4. Uangalizi wa wanyama wanapopata majeraha

Sheria imeanisha kuwa mnyama anaposafirishwa katika chombo cha usafiri na akapata majeraha, inatakiwa kusimamisha safari hiyo na kutoa huduma ya kwanza ili kumsaidia kupata nafuu ya majeraha, pia kutoa taarifa kwa ofisi za serikali mtaa au polisi iliyopo karibu kwa msaada zaidi.

### 5. Taratibu za huduma za upasuaji kwa mnyama

Sheria imeanisha taratibu za kufanya kwa mnyama wakati anapofanyiwa huduma za upasuaji ikiwa ni pamoja na kumchoma sindano ya kumuondolea maumivu au kutumia dawa ya usingizi na huduma hii itatolewa na mtaalam wa wanyama aliesajiliwa kwa usalama wa afya.

### 6. Kumtunza mnyama asiye na makazi

Ikiwa mnyama anateseka mahali, sheria inakuruhusu umtaarifu kiongozi wa lile eneo ili akupe kibali cha kumchukua na kumtunza mnyama huyo ambapo mmiliki wake atakamatwa na kurejesha gharama zote za matunzo ikiwa atahitaji kumchua mnyama au mfugo wake.

## Makosa

Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria kwa kufanya vitendivifuatavyo kwa mnyama;

(a) Kumpiga, kumtesa, kumzidishia kumbebesha mizigo mizito mnyama;
(b) Kumnyima chakula au kumpa chakula kiasi kidogo, maji;
(c) Kumuweka mnyama katika mazingira machafu;
(d) Kumtelekeza mnyama na kumsababishia mateso;
(e) Kumuweka au kumtunza mnyama katika mazingira yakumuondolea uasili wake
(f) Kusaidia utesaji wa wanyama;
(g) Kumbeba mnyama katika mazingira yatakayo msababishia maumivu; na
(h) Kuweka mazingira ya wanyama kupigana au kuumizana.

## Adhabu

Sheria imeainisha adhabu kwa mtu yoyote ambaye atafanya kosa la kupiga, kuumiza wanyama au kuwatesa wanyama kwa namna yoyote ikithibitika atapewa adhabu ya kulipa faini isiyopungua laki moja na isiyozidi milioni moja au kifungo.

## Hitimisho

Ustawi wa wanyama ni jambo muhimu kwa jamii yoyote kwa kuwa ni viumbe hai. Wanyama wanafaida kubwa katika uchumi wa Tanzania. Sheria hii inalenga katika kuhakikisha wafugaji wa wanyama na jamii kwa ujumla zinatekeleza wajibu wao ipasavyo.

---

**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv

**JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



# SHERIA YA USTAWI WA WANYAMA

# SHERIA YA USTAWI WA WANYAMA

## 1. 0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980, kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kuanzishwa kwa sheria hizo yanafikiwa. Aidha Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki katika maboresho ya sheria.

Kutokana na umuhimu wa sekta ya mifugo katika jamii za kitanzania Serikali ilitunga Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154.

## 2.0 SHERIA YA USTAWI WA WANYAMA

Kwa kuzingatia sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154 wanyama wanaofugwa na binadamu wanastahili kupata huduma muhimu kama viumbe hai ambavyo vina thamani kubwa kwa binadamu.

### Masuala ya kuzingatia katika ustawi wa wanyama

Kwa kuzingatia kanuni na msingi wa Sera ya Taifa ya Mifugo na Ustawi wa Wanyama, Sheria inaelekeza masuala muhimu ya kuzingatia katika ustawi wa wanyama kama ifuatavyo;

(i). Kuhakikisha kwamba wanyama wanatunzwa katika mazingira mazuri na salama;
(ii). Wanyama wanapewa chakula au malisho bora,
(iii). Wanyama wanatunzwa na kuwaepusha dhidi ya maumivu, majeraha na magonjwa.

**Haki za wanyama.**
Sheria ya Ustawi wa Wanyama Sura ya 154 imeainisha haki za manyama kama ifuatavyo;

**(i) Haki ya kutunzwa**
Mnyama ana haki ya kutunzwa hivyo mfugaji anawajibika kumtunza vizuri mnyama wake ikiwa ni pamoja na kumpa chakula, banda ambalo litamkinga dhidi ya mvua na jua na liwe mwanga wa kutosha.

**(ii) Haki ya matibabu**
Mnyama ana haki ya kupata matibabu,na mfugaji anatakiwa kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na mtaalam wakati wote wa matibabu hayo.

**(iii) Kuishi maisha ya asili**
Wanyama wote wanastahili kupata nafasi ya kutosha kuishi maisha ya asili katika mazingira yake ya asili.

### Kamati ya ushauri wa ustawi wa mnyama

Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154 imeanzisha Kamati ya Ushauri wa ustawi wa mnyama, Kamati hii ina jukumu la kumshauri waziri mwenye dhamana ya masuala ya mifugo kuhusu masuala yote yanayohusu ustawi wa mnyama.

### Wajibu wa Mkaguzi wa ustawi wa mnyama

Sheria ya Ustawi wa Wanyama imeanisha uwepo wa wakaguzi. Wakaguzi wana majukumu yafuatayo;-

(i). Kuhakikisha kuwa mnyama anaesafirishwa awe na afya na apewe huduma ya chakula,maji na hewa safi wakati wote wa safari mpaka atakapofika;
(ii). Kuhakikisha mnyama anachinjwa kwa kuzingatia uangalizi na mazingira yasiyo ya mateso kwa matumizi ya chakula na biashara;
(iii). Kuhakikisha mnyama anakuwa na uangalizi mzuri wakati wa shughuli za matumizi kama vile kazi, michezo au katika maabara za wanyama; na
(iv). Kuhakikisha mnyama anatunzwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na tartibu zilizowekwa.

### Mamlaka ya Mkaguzi wa Ustawi wa Mnyama

Sheria ya ustawi wa mnyama imeainisha mamlaka mkaguzi wa ustawi wa wanyama kama ifuatavyo;

i). Kuingia na kukagia chombo chochote cha usafiri, nyumba ambayo anahisi au kwa kujua kuwa kinasafirisha mnyama
ii). Kumtaka mmiliki au msimamizi wa chombo cha usafiri au nyumba kuweka mazingira bora ya kusafirisha au kumtunza mnyama
iii). Kumkabidhi polisi au kwa mwendesha mashtaka mtu yeyot ambaye atakiuka sheria ya ustawi wa mnyama.
iv). Kufanya uchunguzi kuhusiana na mtu yeyote atayekuwa amekiuka vigezo vilivyowekwa na sheria kwa ustawi wa mnyama.

### Wajibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

i) Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154 imezipa mamlaka za Serikali za Mitaa za kutengeneza sheria ndogo ambazo zitasimamia ustawi mnyama katika maeneo yao ya utawala.
ii) Kuanzisha au kuruhusu sekta binafsi au mashirika ya kijamii kuomba kibali cha kuanzisha vituo vya kutoa huduma kwa mnyama wasio na makazi maalumu au waliotelekezwa pale anapohitaji huduma za uangalizi wa matibabu kwa mnyama mwenye majeraha au alieugua.

iii) Kufanya utaratibu wa haraka wa kuondoa mwili wa mnyama aliekufa katika miundombinu ya barabara na kumzika ili kuepusha madhara ya kiafya nauchafuzi wa mazingira.

### Mamlaka ya Kufanya Uchunguzi

Sheria ya Ustawi wa Mnyama Sura ya 154 imempa mamlaka Mkurugenzi wa Ustawi wa Wanyama pale inapotokea Sheria ya Ustawi wa Wanyama imekiukwa kufanya uchunguzi na kufungua malalamiko kutokana na taarifa ya kiuchunguzi na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

### Mamlaka ya Waziri ya kutunga Kanuni

Sheria ya Ustawi wa Mnyama imempa mamlaka waziri mwenye dhamana na masuala ya wanyama kutengeneza kanuni pale ataoona inafaa kwa ustawi na utekelezaji mzuri wa sharia ya ustawi wa wanyama.

### Mazingira ya ustawi wa wanyama

Sheria ya Ustawi wa Mnyama Sura 154 imeainisha mazingira ambayo mnyama anakiwa kuwekewa kwa ustawi kama ifuatavyo;

**1. Matunzo bora**
Sheria inaelekeza kuweka ambayo mnyama anatunzwa katika mazingira safi na salama; Wanyama wanapewa chakula au malisho anayostahili, anaishi katika mazingira safi.

**2. Usafirishaji wanyama**
Ili kulinda ustawi wa wanyama sheria imekataza kusafirisha wanyama kwa namna ambayo mnyama atakuwa katika mazingira magumu ya kuteseka au kuumizwa wakati wa kumsafirisha. Mnyama anatakiwa kusafirishwa katika mazingira salama bila kubugudhiwa.